

AHMES SECONDARY SCHOOL
KIDATO CHA KWANZA TARAJALI, MAZOEZI WAKATI WA LIKIZO 2021
MAARIFA YA KIISLAMU

TAWHIID SEHEMU A.

Jibu maswali yote.

1. (a) Eleza kwa kifupi neno Tawhiid maana yake:
 - (i) Kilugha.
 - (ii) Kisheria
- (b) Taja aina kuu tatu za Tawhiid na zielezee kwa kifupi sana.
2. (a) Nini maana ya Elimu katika uislamu ?
- (b) Ni nani alieelimika ? Toa sifa za mtu aliyeelimika.
- (c) *".....Sema, Je, wanaweza kuwa sawa wale wanaojua na wale wasiojua? Wanaotanabahi ni wale wenye akili tu." (39:9)*

Toa maoni juu ya aya hii jee ni upi umuhimu wake ?

- (d) *"Mfano wa wale waliopewa Taurati kisha hawakuichukua (kwa kuitia katika matendo) ni kama punda aliyebeba (mzigo) wa vitabu vikubwa (bila ya kufaidika kwavyo) ni mbaya kabisa mfano wawatu waliokadhibisha aya za Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu madhalimu." (62:5).*

Ni watu gani wanaopigwa mfano katika Aya hii ya Qur'ani ?

3. Toa mafunzo matano yanayopatikana ndani ya Qur'ani (96:1-5)

4.(a) Unaelewa nini kuhusu aya hii ?

"..... Kwa hakika wanaomuogopa Mwenyezi Mungu miongoni mwa waja wake ni wale wataalam (waliozama katika fani mbali mbali)....." (35:28).

(b) Elezea umuhimu wa Aya hii katika Elimu.

".....Hakika swala humzuilia (mja) na mambo machafu na maovu na ni dhikri kubwa kwa Allah (s.w)....." (29:45).

(c) Nini kinachosisitizwa katika ayah hii kuhusu Elimu ?

".....Mwenyezi Mungu atawainua (daraja) wale walioamini miongoni mwenu, na waliopewa elimu watapata daraja zaidi"(58:11)

(d) *"Katika kuumbwa mbingu na ardhi na mfuatano wa usiku na mchana, ziko hoja (za kuonesha kuwepo Allah(s.w) kwa wenye akili. (3:190) Ambao humkumbuka Mwenyezi Mungu wakiwa wima, wakiwa wamekaa na wakiwa wamelala. Na hufikiri (tena) umbo la mbingu na ardhi (wakasema) Mola wetu! Hukuviumba hivi bure bure tu. Utukufu ni wako. Basi tuepushe na adhabu ya moto." (3:191)*

Toa maoni yako ayah hizi zina umuhimu gani kwa mwanadamu kuzifahamu ?

5. (a) Na haikuwa kwa mtu kwamba Mwenyezi Mungu anasema naye ila kwa il-hamu (anayetiwa moyoni mwake) au kwa nyuma ya pazia au humtuma mjumbe (Malaika) naye humfunulia kiasi anachotaka kwa idhini yake (Allah), bila shaka yeye ndiye aliye juu mwenyehakima." (42:51).

Taja njia tatu za kujipatia Elimu zilizotajwa katika ayah hii, Pia Ni Nani chanzo cha Elimu ?

(b) Taja njia nyingine zilizobaki ambazo hutumika vilevile kufikisha Elimu kwa waja wa Allah

6. (a) Naapa kwa nyota zinapoanguka. (Zinapokuchwa). Kwamba mtu wenu (huyu Muhammad) hakupotea kwa ujinga wala hakukosa. (na hali ya kurwa anajua); wala hasemi kwa matamania (ya nafsi yake). (53:1-3)

(i) Ni njia gani ya Elimu inayotakaswa katika ay hii ?

(ii) Ni malaika gani anaetamkwa hapa ?

(b) Tofautisha kati ya Elimu Maarifa na Elimu mwongozo.

(c) Toa maana ya Elimu yenye manufaa.

7. Kwa ushahidi wenye mifano hai Toa sababu tano kwa nini Uislamu haukubali mgawanyo wa Elimu Dunia na Elimu Akhera.

8. Toa maelezo yenye ushahidi wa Qur'an kuonesha kuwa:

(a) Elimu ndiyo takrima ya kwanza aliyotunukiwa binadamu na Mola wake.

(b) Kutafuta elimu kwa ajili ya Allah(s.w) ni faradh ya kwanza kwa Waislamu.

(c) Kwa kurejea Qur'an oneshwa kuwa katika Uislamu kuna:

(i) Elimu ya Mwongozo.

(ii) Elimu ya Mazingira.

9. (a) Maana ya Dini kwa Mtazamo wa Makafiri ni _____

(b) Maana ya Dini kwa Mtazamo wa Uislamu ni _____

(c) Hapa Ulimwenguni kuna Dini kubwa mbili ambazo ni:-

(i) _____

(ii) _____

10. (a) "Je, Wanataka Dini isiyokuwa ya Mwenyezi Mungu na hali kila kilichomo mbinguni na ardhini kimejisalimisha kwake kipende kisipende. Na kwake Mtarejeshwa wote" (3:83).

Kwa kuzingatia aya hii toa mafunzo mawili (2) yanayohusiana na Dini.

(b) (i) Toa maana mbili za neno "Islam".

(ii) Nani Muislamu?

(c) Tofautisha katik ya Muislamu na Muumini kwa mazingatio ya Ayah ya hapa chini.

"Walisema wanaoaka Jangwani "Tumeamini" sema (Uwaambie) Hamjaamini (kweli kweli bado) lakini semeni, tumesilimu, maana Imani haijaingia vyema nyoyoni mwenu bado....." (49:14).

11. (a) "Hautokei msiba katika ardhi wala katika nafsi zenu ila umekwishaandikwa katika kitabu (cha Mwenyezi Mungu) kabla hatujaumba. Kwa yakini hilo ni sahali kwa Mwenyezi Mungu" (57:22).

Ayah hii inaonesha nguzo gani ya imani ?

(b) (a) Nini maana ya "Imani"?

(c) Orodhesha nguzo za Imani ya Kiislamu zilizotajwa katika Qur'an (2:285).

(d) Kuamini Qadar ya Allah ni kuamini kuwa.....

(e) Orodhesha sifa za Waumini zilizobainishwa katika aya zifuatazo: (i) (8:2-4). (ii) (23:1-11).

(f) Na katika watu wako wasemao tumemuamini Allah na siku ya Mwisho na hali ya kurwa si wenye kuamini" (2:8).

Pamoja na kudai kwao kuwa ni waumini, Allah(s.w) anatumfahamisha kuwa hawajaamini, kwa nini?

MWISHO.

Maswali haya yafanyike yote kwenye daftari na yatakaguliwa inshaallah.